

## TABLE OF CONTENTS

## Page

Notice of the 2006 Annual General Meeting	2
Chairman's Report	3 - 4
Managing Director's Report	5 - 10
Board of Directors	11 - 12
Shareholding structure	13
Corporate Information	14
Directors report	15
Statement of Directors' Responsibilities	16
Report of the Independent Auditors	17
<b>Financial statements:</b>	
Profit and loss account	18
Balance sheet	19
Statement of changes in equity	20
Cash flow statement	21
Notes	22 – 37
Five Year Financial Record	38
Proxy Form	39

## NOTICE OF THE ANNUAL GENERAL MEETING

**NOTICE IS HEREBY** given that the 40th Annual General Meeting of the Members will be held at the Company's Factory Premises George Morara Avenue, Nakuru on Thursday, 22nd March 2007 at 12.00 noon for the following purposes:-

1. To confirm the minutes of the 39th Annual General Meeting held on 14th December, 2005;
2. To receive, consider and if deemed fit, adopt the financial statements for the year ended 30th September, 2006 together with the reports thereon of the Directors and of the Auditors.
3. To declare a final dividend of Shs. 0.60 per share.
4. a) To elect Directors:
  - i) ICDC, a director retiring by rotation, which being eligible, offers itself for re-election.
  - ii) M. H. Da Gama-Rose, a director retiring by rotation, who being eligible, offers himself for re-election:
- b) Special notice is hereby given pursuant to Section 186(5) of the Companies Act, to consider the following resolution:

“That Mr. M. H. Da Gama-Rose a director who has attained the age of 76 years, be and is hereby re-elected a director of the Company.”
5. To confirm the Directors' emoluments.
6. To appoint PricewaterhouseCoopers as auditors for the ensuing year and to authorize the Directors to fix the auditors remuneration.
7. To transact any other business which may be transacted at an Annual General Meeting.

### By Order of the Board

**Issa Timamy**  
**Company Secretary**  
**Nairobi**

19 December 2006

Notes:

A member entitled to attend and vote at this meeting may appoint a proxy to attend and vote on his/her behalf and such a proxy need not be a member of the Company. The form of proxy is attached on page 39.

The final dividend, if approved, will be paid on or about 30th March, 2007 to members on the register at close of business on 9th February, 2007.

## **CHAIRMAN'S REPORT**

Chairman's message to shareholders,

First, I would like to welcome our new shareholders. We now have over 175,000 shareholders after completing the most successful IPO in Kenya's history. This shows the overwhelming support for our Company and the faith many have in the future of Eveready.

From where I sit; our Company has a proud past and bright future. Later in the annual report our Managing Director, Mr. Steven G. Smith will go into the details about our 2006 business year and what to expect for the future. I would like to discuss our Company from a Board view point.

We will be expanding director positions in 2007 with two independent directors in addition to the current seven directors we have. We have a strong Board and Management team that has always directed this Company in a fully transparent manner with a view for growth in a challenging business environment. The new directors will strengthen our Board and offer additional resources for Eveready's Management team to draw upon.

Our product lines continue to expand for Eveready. We now offer in Kenya personal care products (Schick) and have continued to expand our battery and flashlight ranges. We are the only company that can meet all your portable battery needs. We see the needs of the consumer changing and we also have rechargeable batteries and the world's longest lasting AA battery for the new digital devices.

We are also focused on improvements at our factory. We have access to leading technology and support for our equipment from Eveready Battery Company, USA. Our factory continues to manufacture "D" batteries of the technology required by the East African consumer; who ask for low prices and these batteries represents more than 75% of batteries sold in East Africa. We have excellent quality and prices that give the consumer a choice with our products. While our prices are not the lowest; our products exceed all the safety and quality standards required. Many of the various competing brands with lower prices will not pass the Kenya Bureau of Standards requirements or IEC requirements. Our products will meet and exceed these standards every time. Substandard batteries must be stopped by the Government and we have continuous dialogue with various agencies in the Government regarding this matter. I however encourage you to support local industries and buy "Kenyan" whenever possible.

When the consumer is able to move away from the current "D" battery construction type we will also have the ability to change our manufacturing equipment because of the relationship we have with Eveready Battery Company, USA. We will be ready for the future. Our Company is already reaching out to other East African countries for top line sales growth and is ready to meet the AA battery growth we see for the future.

Our products are recognized for "proven value" and "trusted quality" in Kenya and we all need to promote our brands – Eveready, Energizer and Schick with families and friends. I encourage all shareholders to attend our Annual General Meeting on March 22, 2007 in Nakuru. The directors, company officers and I look forward to building our relationship and I thank you in advance for your cooperation and support of our company.

**Naushad N. Merali, CBS**

**Chairman**

**December 19, 2006**

## **UJUMBE WA MWENYEKITI KWA WENYEHISA**

Kwanza, ningependa kuwakaribisha Wenyehisa wetu wapya. Kwa sasa tuna zaidi ya Wenyehisa 175 elfu baada ya kukamilisha uuzaji uliofaulu wa tolea la kwanza la hisa katika historia ya Kenya. Hii inaonyesha jinsi kampuni yetu inavyoingwa mkono na wengi na imani waliyo nayo wengi kwa kampuni ya Eveready kwa siku zijazo.

Kuanzia mahali ninapokaa, kampuni yetu inajivunia wakati uliopita na matarajio mema siku zijazo. Baadaye katika taarifa ya kila mwaka Mkurugenzi wetu Mkuu, Bwana Steven G. Smith ataelezea zaidi kuhusu biashara yetu mwaka wa 2006 na kile tunachotarajia kwa siku zijazo. Ningependa kujadili kuhusu kampuni yetu kuanzia maoni ya Halmashauri.

Tutaongeza nafasi za wakurugenzi mwaka wa 2007 huku kukiwa na wakurugenzi wawili huru kuongezea idadi ya wakurugenzi saba tulio nao kwa sasa. Tuna Halmashauri yenye nguvu na kundi la Wasimamizi ambalo kila mara limeielekeza kampuni hii kwenye mkondo kamili wa uwazi kwa lengo la kukuza shughuli za biashara yake katika mazingira ya kibiashara yenye changamoto kubwa. Wakurugenzi wapya wataimarisha Halmashauri yetu na kutoa rasilimali zaidi kwa kundi la usimamizi wa kampuni ya Eveready kuimarisha biashara yake.

Laini zetu za utoaji bidhaa zaendelea kupanuka kwa Eveready. Kwa wakati huu hapa nchini tunatoa bidhaa za ulinzi wa kibinafsi (Shick) na tumeendelea kupanua bidhaa za betri na tochi. Tuna kampuni ya pekee inayoweza kutimiza mahitaji yako yote ya betri ndogo. Tunaona haja ya kubadilika kwa matumizi ya wateja na pia tuna betri za kuweka chaji, yaani unazoweza kuongeza nguvu na betri zinazokaa kwa muda mrefu sana aina ya AA kwa mitambo ya kisasa ya dijitali.

Pia tunazingatia uboreshaji wa kiwanda chetu. Tunapata teknolojia za hali ya juu na msaada kutoka kwa kiwanda chetu kampuni ya Eveready Battery cha Marekani. Kiwanda chetu kinaendelea kutengeneza betri za kiwango “D” za teknolojia inayohitajika kwa wateja wa Afrika Mashariki wanaohitaji betri za bei nafuu na za aina hii ambazo zinawakilisha zaidi ya asilimia 75 ya betri zinazouzwa sasa katika eneo la Afrika Mashariki. Tuna bidhaa bora na za bei nzuri zinazowapatia wateja chaguo la bidhaa zetu. Huku ikiwa bei zetu si za chini sana, zinafikia viwango vyote vya usalama na ubora unaohitajika. Nyingi ya bidhaa mbali mbali za bei nafuu hazitimizi viwango vya ubora vinavyohitajiwa na Shirika la Ukadiriaji ubora wa bidhaa nchini KBS au IEC. Bidhaa zetu zinatimiza na kupita viwango hivi kila wakati. Betri za viwango duni lazima zikomeshe na Serikali na tunafanya mashauri kila mara na mashirika mbali mbali ya serikali kuhusiana na swala hili. Hata hivyo nimewahimiza kuunga mkono viwanda vya humu nchini na kununua bidhaa za Kenya’ ikiwezekana.

Wakati wateja watakapoweza kubadili matumizi ya aina ya sasa ya betri za kiwango “D” pia nasi tutakuwa na uwezo wa kubadili mtambo wetu wa kutengeneza bidhaa mpya kwa sababu ya uhusiano mwema kati yetu na kampuni ya Eveready Battery ya Marekani. Tutakuwa tayari kwa siku zijazo. Kampuni yetu tayari inafikia nchi nyingine za Afrika Mashariki kwa kiwango cha juu cha ukuaji wa mauzo na iko tayari kutimiza mahitaji yanayoongezeka ya betri za kiwango cha AA siku zijazo.

Bidhaa zetu zinatambuliwa kwa “thamani iliyothibitishwa” na “ubora wa kuaminika” hapa nchini na sote tunahitajika kutangaza bidhaa zetu – Eveready, Energizer na Schick pamoja na familia na marafiki. Nina wahimiza Wenye-hisa wote kuhudhuria mkutano wetu mkuu wa kila mwaka tarehe 22 Machi, 2007 huko Nakuru. Wakurugenzi, maafisa wa kampuni pamoja nami tunatazamia kujenga uhusiano wetu na nawashukuru kwa ushirikiano wenu na msaada wa kampuni yetu.

**Naushad N. Merali, CBS**

**Mwenyekiti**

**Desemba 19, 2006**

## **UJUMBE WA MWENYEKITI KWA WENYEHISA**

Kwanza, ningependa kuwakaribisha Wenye-hisa wetu wapya. Kwa sasa tuna zaidi ya Wenye-hisa 175 elfu baada ya kukamilisha uuzaji uliofaulu wa tolea la kwanza la hisa katika historia ya Kenya. Hii inaonyesha jinsi kampuni yetu inavyoingwa mkono na wengi na imani waliyo nayo wengi kwa kampuni ya Eveready kwa siku zijazo.

Kuanzia mahali ninapokaa, kampuni yetu inajivunia wakati uliopita na matarajio mema siku zijazo. Baadaye katika taarifa ya kila mwaka Mkurugenzi wetu Mkuu, Bwana Steven G. Smith ataeleza zaidi kuhusu biashara yetu mwaka wa 2006 na kile tunachotarajia kwa siku zijazo. Ningependa kujadili kuhusu kampuni yetu kuanzia maoni ya Halmashauri.

Tutaongeza nafasi za wakurugenzi mwaka wa 2007 huku kukiwa na wakurugenzi wawili huru kuongezea idadi ya wakurugenzi saba tulio nao kwa sasa. Tuna Halmashauri yenye nguvu na kundi la Wasimamizi ambalo kila mara limeielekeza kampuni hii kwenye mkondo kamili wa uwazi kwa lengo la kukuza shughuli za biashara yake katika mazingira ya kibiashara yenye changamoto kubwa. Wakurugenzi wapya wataimarisha Halmashauri yetu na kutoa rasilimali zaidi kwa kundi la usimamizi wa kampuni ya Eveready kuimarisha biashara yake.

Laini zetu za utoaji bidhaa zaendelea kupanuka kwa Eveready. Kwa wakati huu hapa nchini tunatoa bidhaa za ulinzi wa kibinafsi (Shick) na tumeendelea kupanua bidhaa za betri na tochi. Tuna kampuni ya pekee inayoweza kutimiza mahitaji yako yote ya betri ndogo. Tunaona haja ya kubadilika kwa matumizi ya wateja na pia tuna betri za kuweka chaji, yaani unazoweza kuongeza nguvu na betri zinazokaa kwa muda mrefu sana aina ya AA kwa mitambo ya kisasa ya dijitali.

Pia tunazingatia uboreshaji wa kiwanda chetu. Tunapata teknolojia za hali ya juu na msaada kutoka kwa kiwanda chetu kampuni ya Eveready Battery cha Marekani. Kiwanda chetu kinaendelea kutengeneza betri za kiwango “D” za teknolojia inayohitajika kwa wateja wa Afrika Mashariki wanaohitaji betri za bei nafuu na za aina hii ambazo zinawakilisha zaidi ya asilimia 75 ya betri zinazouzwa sasa katika eneo la Afrika Mashariki. Tuna bidhaa bora na za bei nzuri zinazowapatia wateja chaguo la bidhaa zetu. Huku ikiwa bei zetu si za chini sana, zinafikia viwango vyote vya usalama na ubora unaohitajika. Nyingi ya bidhaa mbali mbali za bei nafuu hazitimizi viwango vya ubora vinavyohitajiwa na Shirika la Ukadiriaji ubora wa bidhaa nchini KBS au IEC. Bidhaa zetu zinatimiza na kupita viwango hivi kila wakati. Betri za viwango duni lazima zikomeshe na Serikali na tunafanya mashauri kila mara na mashirika mbali mbali ya serikali kuhusiana na swala hili. Hata hivyo nimewahimiza kuunga mkono viwanda vya humu nchini na kununua bidhaa za Kenya’ ikiwezekana.

Wakati wateja watakapoweza kubadili matumizi ya aina ya sasa ya betri za kiwango “D” pia nasi tutakuwa na uwezo wa kubadili mtambo wetu wa kutengeneza bidhaa mpya kwa sababu ya uhusiano mwema kati yetu na kampuni ya Eveready Battery ya Marekani. Tutakuwa tayari kwa siku zijazo. Kampuni yetu tayari inafikia nchi nyingine za Afrika Mashariki kwa kiwango cha juu cha ukuaji wa mauzo na iko tayari kutimiza mahitaji yanayoongezeka ya betri za kiwango cha AA siku zijazo.

Bidhaa zetu zinatambuliwa kwa “thamani iliyothibitishwa” na “ubora wa kuaminika” hapa nchini na sote tunahitajika kutangaza bidhaa zetu – Eveready, Energizer na Schick pamoja na familia na marafiki. Nina wahimiza Wenye-hisa wote kuhudhuria mkutano wetu mkuu wa kila mwaka tarehe 22 Machi, 2007 huko Nakuru. Wakurugenzi, maafisa wa kampuni pamoja nami tunatazamia kujenga uhusiano wetu na nawashukuru kwa ushirikiano wenu na msaada wa kampuni yetu.

## **MANAGING DIRECTOR'S REPORT**

Our products – Eveready, Energizer and Schick are used by many through out East Africa and how the consuming public reacts to the challenges they encounter will have an impact on our company success. We estimate that we have approximately 5 million consumers using our products every month. However, if we have a drought or floods in Kenya we will see the negative impact very quickly in our sales; just as when the government correctly enforces standards; we see the positive impact on our sales. Many Eveready consumers in 2006 did not see their disposable income increase and were also impacted by higher food prices and oil related price increases in 2006. The Company was also impacted by significant raw material price increases. Zinc cost increased almost three times in 2006. However, when I review the entire year we were successful and actually improved our overall position by the actions we have taken. With the declining economic trends during the first half of 2006; we reduced the price of our 950 blue product which reduced our income by KShs 20 million but helped consumers to continue to use our products.

### **Safety, Health and Environment Review**

At Eveready, we believe that our colleagues are our most important asset and that their Safety and Health is our greatest responsibility. We strive to meet or exceed all Kenya standards as well as internal standards of Eveready Battery Company, USA (EBC). Training is periodically provided by EBC and audits are conducted to confirm appropriate program management and to identify opportunities to further improve.

During 2006 we completed the closing of all waste disposal sites on our property. While not required by Kenyan law it was the correct thing to do. This project cost us KShs 9 million and will not re-occur in 2007. In 2007 we plan to remove all under ground storage tanks to meet Eveready's goals of eliminating the potential for environmental impact. We also have in place a zero waste water discharge program at our factory. No water that is used in our manufacturing process leaves our facility. It is recycled onsite and used back into our process. We also apply this to solid waste and encourage recycling of manufacturing waste. We have an activity waste and energy reduction program. On a negative note we had over 20 off-the job injuries in 2006 with most of these accidents being tied to falls and/or vehicles that contributed to over 100 lost work days.

High energy cost continues to affect many; however, for Eveready we have undertaken for years the importance of controlling our energy consumption. Eveready's total energy cost is less than 3.5% of our total manufacturing cost. We also believe this can be reduced and are spending to upgrade various electrical systems. During 2006, we spent over KShs 3.5 Million on these projects; which we will realize the benefits from this investment in the coming years. We will spend additional money on our electrical distribution system in the coming years which will cost approximately KShs 20 million. These upgrades will be driven by improvements in safety and capacity needs but will also offer additional saving in our energy bill.

### **Human Resources Review**

We have over five hundred people working directly for Eveready and do believe this is our most valuable resource. Our distributors directly employ more than 200 people. We currently employ about 130 contract employees along with 370 permanent employees. Approximately 450 people are employed at our operations in Nakuru. We provide various benefits that meet and exceed Kenyan law for all employees.

We have a full time doctor at our factory clinic staffed with nurses on two shifts that are available to all employees. Our permanent employees are also provided with medical insurance that makes available more than KShs 200,000 in employee benefits per year. During 2006 we paid over KShs 22 million for medical benefit expenses.

The factory's Safety and Health program is provided with oversight and guidance by the General Safety Committee and a Management Safety, Health and Environmental Committee. These committees help to ensure compliance with the Factories Act, NEMA regulations and the Labor Act. Our Collective Bargaining Agreement with the Kenya Chemical and Allied Workers Union continues to be honored by both sides with the current agreement expiring July 2008.

We believe we have one of the most progressive HIV/AIDS policies in Kenya. Our employees and spouses have free access to testing, counseling and antiretroviral drugs for life. We believe that when people retire from Eveready with HIV/AIDS we should continue to help support them. We have also included with our life insurance benefits; insurance riders which help with critical illness and assist with payment for HIV/AIDS related medical treatment. We also provide HIV/AIDS training for our employees and our employees' children. Last year we saw more than 1,000 children and young adults go through this program sponsored by Eveready. We spent in 2006 about KShs 2.5 million for our various HIV/AIDS programs. For our life insurance programs we spend more than KShs 4.3 million per year in premiums.

Our permanent hourly employees have a gratuity program for retirement and our salary employees have a defined contribution program for retirement. We did close the salary retirement defined benefit program in October 2006 in favor of a defined contribution retirement program. We will continue to fund the retirement defined benefit program for the next three years at a cost of approximately KShs 19 million and after three years we will consider a full conversion to a defined contribution retirement program for benefits earned before October 2006. We contribute approximately 8.5% of our payroll cost to maintain these retirement benefits for our employees.

Our Nakuru factory employees continue to be highest paid for factories in the Nakuru area and are one of the top wage earners when compared to Nairobi factories. Our salaried employees' salary benefits compare favorable with market conditions for the positions they are in.

For our Nakuru operations; we also provide a canteen operation that provides meals to employees. The employee only pays KShs 6 per meal they consume. The operation of this benefits costs the company KShs 8 million per year. We also provide free transport to Nakuru employees who work between 6PM and 6AM. This costs Eveready approximately KShs 5.5 million.

We also believe in training for our employees; which includes training trips to other EBC locations. During 2006 we spent over KShs 5 million for training and developing our future leaders and had more than 75 man days spent at other EBC locations for training. EBC also sends training and technical personnel to Kenya for training and improvement programs that are covered under our technical service agreement. During 2006 EBC provided more than 200 man days of on site assistance in a variety of technical areas. We spent over KShs 300 million for wages, benefits and other employee programs in 2006.

### **Corporate Social Responsibility Review**

We spent about KShs 5 million in programs designed to give back to the community we live and work in. This includes KShs 800,000 spent on children HIV/AIDS education, KShs 1 million for famine relief and KShs 0.5 million for water wells. We also spent approximately KShs 500,000 for various programs designed to help train government

employees on understanding the impact of counterfeit and illegal products. We also supported various programs focusing on children, forest protection and women's issues. We have budgeted to spend approximately KShs 6 million for this area in 2007. This represents approximately 3% of our net income after taxes.

### **Corporate Governance Review**

We have always managed our business in an open and transparent manner. We feel strongly that ethical business practices at all levels of our company is important. If we find an ethical problem it will be discussed with the audit committee and the board which includes actions we take to resolve a situation and where appropriate we will turn over information to legal authorities for possible criminal prosecution.

We will be making changes in Board Member assignments to our Board Committees in 2007 with the addition of two independent directors. The current board committees are:

- Finance & Risk Committee
- Audit Committee
- Remuneration and Nomination Committee

We have in place a Business Practice & Standards of Conduct Policy for all employees and an Insider Trading Rules for all employees which can be found on our web site. These policies also apply to company officers and directors. We also send out annually to all local suppliers our Business Practice Policy for Business Partners and also ask employees to fill out a questionnaire annually confirming business conduct activities have met Eveready's policies during the past year.

We believe strongly in operating our business ethically and that there are "no short cuts". We must do the Right Thing Every Time.

### **Manufacturing Review**

During 2006 we kicked off our Factory Improvement Program. We estimate we will average spending KShs 50 million per year on this program for the next several years. For 2006 we spent in total about KShs 63 million on all capital improvements for the company. Our Factory Improvement Program is divided into three areas: People, System and Equipment. During 2006 we spent a great deal of time on people and system issues. Training and performance evaluation played a major role as we must have the right people with the right education. Using EBC's technical experts we have begun a Lean Manufacturing effort. This has required that we look at our equipment maintenance process and have put in place major preventive maintenance upgrades in 2006 that required a new approach from all in the factory. We also began an equipment overhaul program in several areas.

We also have begun to look at factory operation on a return of installed capacity. We currently only use about 60% of our installed capacity but we have taken this a step further that includes looking at how effective we are in managing the time we have this resource available for use. This says it is important to understand if you have equipment available for 24 hours how well do you use that equipment for the 24 hours vs. historic ways of measuring efficiency.

We have also upgraded several areas in the factory to provide proper resources for our employees. We will spend about KShs 6.5 million on these improvements by the end of 2007.

By far the most important activity in 2007 will be to again address training issues for our factory employees. We must match skills and productivity measures from other EBC factories and work toward global bench marks.

### **Sales & Marketing Review**

During 2006 we did see a decline in total sales mainly due to reasons discussed at the beginning of this report over 2005 results. Our consumers have a preference for low price product and this was reflected in our sales patterns for 2006 along with a price reduction for our 950 blue product.

We do see growth in higher end products for those not affected by crop failures and drought. We also continue to see opportunities for our products in the export markets. We continue to gain market share in both Uganda and Tanzania. However, EAC tax treaty issues continue to favor Tanzania and government failure to enforce standards are problems facing our export business. However overall export business is growing and we will use all product lines to develop these markets. Eveready will be offering portable power solutions for other East African countries this year.

During 2006 we spent over KShs 60 million on advertising and promotion activities. Our programs are designed to segment and give the consumer product options that meet their needs. We are aware of the desire for lower price products; however, if you compare our pricing to other leaders in the battery industry our prices are similar. The pricing issue goes back to illegal products which find their way into Kenya that are under invoiced and have not paid the 16% VAT and 35% import duty in a correct manner. We will continue to investigate these situations and turn over information to government authorities for action.

We will be celebrating our 40th anniversary in 2007 and this will play a part in our promotion activities for 2007.

### **Financial Review**

The year 2006 posed many challenges. There was the drought in the first half of the financial year which led to reduced consumer purchasing power resulting in a decline in the overall battery market. This was compounded by increase in the prices of major raw materials, and in particular, zinc to unprecedented levels and pressure from low cost competition.

Despite these challenges, management instituted appropriate response measures to mitigate the challenges. This was achieved by implementing a competitive pricing strategy in order to maintain our market share position coupled with growth strategies in high performance products and export markets. In addition, management adopted strict control measures over operating costs, during the year. Our corporate overhead expenses were controlled at 2005 levels in 2006.

During 2006 we started the process of integrating and consolidating our computer operation between Nakuru and Nairobi. This included changes in telephone systems which reduced our cost. We expect the computer integration project to be completed by the end of 2007. This will also include an upgrade to our payroll system using BIO technology for factory timecards.

Our sales for 2006 were KShs 2 billion and profit after tax at KShs 166 million compared to KShs 2.2 billion and KShs 187 million respectively in the previous year.

### **Closing Comments**

I am very proud of our company and the growth we have seen in many individuals in 2006. We still have the normal business challenges ahead but, a reduction in our

manufacturing cost is a must. The cost of manufacturing in Kenya remains high when compared to other EBC locations. Our material costs tend to be higher than other EBC locations due to "in country transportation cost" (Mombasa to Nakuru). We are also impacted by the increasing amount of taxes on our company that are not applied in other countries.

For 2006, we had the added burden of a significant increase of zinc prices from US\$ 1,700 to over US\$ 4,000 per ton which represents 30% of a battery's cost. We were not able to increase our prices enough to recover this zinc price increase and had to absorb over KShs 30 million of this increase within the company. Whether competition is legal or illegal; it is competition and we must react in a manner that protects our long term business goals. We will continue to ask the government for a fair and ethical business environment.

We have no changes in the legal claims we are involved in and described in our prospectus. We continue to believe we will have no liability for these health and employment cases. Many of the cases have been delayed by the courts or by plaintiffs during 2006. We feel strongly about our position and our lawyers continue to feel we have a good chance for success in all these claims and accordingly, no contingent liability has been set aside for the claims. We carry employer's liability insurance for the health and safety claims. We have no insurance for employment claims that amount to KShs 163 million for cases that go back to 1995.

Our focus for 2007 is growing the top line sales for bottom line improvement. We are very clear we must support you with proper income performance year to year. We do ask for your support and this means having family and friends to use our products. This also says it is important to use products made in Kenya if they are available from local manufacturers. We are developing several local Kenyan suppliers to supply various raw materials we have been importing for years and expect to have these Kenyan companies fully certified by the end of 2007 to supply Eveready and if they have the capacity they will be able to supply EBC.

I thank the Chairman, directors, shareholders and all my colleagues at Eveready East Africa Ltd. for their cooperation and support in 2006. We at Eveready welcome our new shareholders and look forward to working with you in building our company in 2007.

**Steven George Smith**  
**Managing Director**  
**December 19, 2006**

## **MKURUGENZI MKUU**

Bidhaa zetu za Eveready, Energizer na Schick hutumiwa na wengi kote katika eneo la Afrika Mashariki na jinsi umma unavyotoa maoni mbali mbali kuhusu changamoto wanazokumbana nazo kuna umuhimu mkubwa kwa ufanisi wa kampuni yetu. Tunakisia kwamba tuna takribani wateja milioni 5 watumia bidhaa zetu kila mwezi. Hata hivyo tunapokabiliwa na ukame au mafuriko humu nchini tutaathiriwa kwa haraka katika mauzo yetu, hasa wakati serikali inapohimiza kuzingatiwa kwa viwango vinavyokubaliwa tunapata ufanisi bora kwenye mauzo yetu. Wateja wengi wa bidhaa za Eveready mwaka wa 2006 hawakushuhudia mapato yao ya ununuzi yakiongezeka na pia waliathiriwa na bei za juu za vyakula na ongezeko la bei za mafuta mwaka wa 2006. Kampuni pia iliathiriwa na ongezeko la bei ya mali ghafi. Gharama ya Zinki iliongezeka karibu mara tatu kuliko bei ya kawaida mwaka 2006. Hata hivyo ninapouchunguza mwaka mzima, tulipata ufanisi na hasa kuboresha nafasi yetu kwa ujumla kwa hatua tulizochukua. Kufuatia kudidimia kwa shughuli za kiuchumi wakati wa nusu ya kwanza ya mwaka 2006, tulipunguza bei ya bidhaa ya 950 blue' iliyopunguza mapato yetu kwa shilingi milioni 20 lakini tukawasidia wateja kuendelea kutumia bidhaa zetu.

### **Usalama, Afya na Mazingira**

Katika kampuni ya Eveready tunaamini kwamba wenzetu ni rasilimali muhimu kwetu na kwamba Usalama na Afya yao ni jukumu letu kuu. Tunajitahidi kutimiza au kuendeleza viwango vyote vya Kenya na vile vile vya kampuni ya Eveready Battery ya Marekani (EBC). Mafunzo hutolewa mara kwa mara na EBC na ukaguzi wa hesabu za pesa hufanywa ili kuthibitisha usimamizi bora wa miradi na kutambua sehemu zinazohitaji kuboreshwa zaidi.

Mnamo mwaka 2006 tulikamilisha hatua ya kufunga sehemu zote za uondoaji taka kwenye kiwanda chetu. Huku likiwa si hitaji kubwa la kisheria humu nchini, lilikuwa jambo lifaalo kutekelezwa. Mradi huu ulitugharimu shilingi milioni 9 na hautazinduliwa tena mwaka 2007. Mwaka 2007 tunapanga kuondoa tangi zote za chini ya ardhi ili kutimiza malengo ya kampuni ya Eveready ya kuondoa uwezekano wa kuwoko kwa athari za kimazingira. Pia tuna mradi wa uondoaji maji taka usio na athari zozote kimazingira kwenye kiwanda chetu. Hakuna maji yanayotumika katika mpango wa utengenezaji bidhaa yanayoondolewa kwenye kiwanda chetu. Maji hayo husafishwa papo hapo na kutumiwa kwa shughuli nyingine kwenye kiwanda hicho. Sisi pia hutumia mtindo huu kwa taka nyingine na kuhimiza matumizi ya taka hizo kwa shughuli nyingine. Tuna mradi wa kupunguza taka na kawi. Tukigusia hatari za kazi yetu, tulikuwa na majeruhi 20 nje ya kazi mwaka wa 2006 huku nyingi ya ajali hizi zikihusisha watu kuanguka na magari yaliyochangia kupotea bure kwa siku 100 bila kazi.

Gharama ya juu ya kawi inaendelea kuathiri wengi, hata hivyo kwa kampuni ya Eveready tumezingatia kwa miaka kadhaa umuhimu wa kuthibiti matumizi yetu ya kawi. Jumla ya gharama ya kawi ya Eveready ni chini ya asilimia 3.5 ya jumla ya gharama yetu ya utengenezaji bidhaa. Pia tunaamini gharama hii inaweza kupunguzwa na tunajitahidi kuimarisha vifaa vinavyotumia umeme. Katika mwaka 2006 tulitumia zaidi ya shilingi milioni 3.5 kwa miradi hii itakayoleta manufaa kutokana na uwekezaji huu katika miaka ijayo. Tutatumia pesa zaidi kwenye vifaa vyetu vinavyotumia umeme katika miaka ijayo kwa gharama ya shilingi milioni 20. Uboreshaji huu wa vifaa utaimarisha usalama na kiwango cha mahitaji lakini utaokoa malipo ya kawi yetu.

### **Wafanyikazi**

Tuna zaidi ya wafanyikazi mia tano wanaofanyikazi moja kwa moja na kampuni ya Eveready na tunaamini hawa ndio rasilimali yetu muhimu. Wagawaji wa bidhaa zetu wamewaajiri moja kwa moja zaidi ya watu 200. Kwa wakati huu tumewaajiri kwa kandarasi wafanyikazi 130 pamoja na wafanyikazi 370 wa kudumu. Tuna takriban watu 450 walioajiriwa kuendesha shughuli zetu mbali mbali huko Nakuru. Sisi hutoa manufaa mbali mbali yanayotimiza na kupita sheria ya Kenya kwa wafanyikazi wote.

Tuna daktari anayehudumu wakati wote kwenye Kliniki ya kiwanda chetu akiwa na wauguzi kwa zamu mbili za wafanyikazi wetu wote. Wafanyikazi wetu wa kudumu pia wanawekewa bima ya matibabu inayotoa shilingi elfu 200 kama marupurupu ya mfanyikazi kila mwaka. Mnamo mwaka 2006 tulilipa zaidi ya shilingi milioni 22 kama gharama za marupurupu ya matibabu.

Mradi wa Usalama na Afya wa kiwanda chetu unazingatiwa na kupata mwongozo wa kamati Kuu za Usalama na Usimamizi, Afya na Mazingira. Kamati hizi husaidia kuhakikisha uzingatiwa wa sheria za viwanda, sheria za Halmashauri ya kitaifa ya usimamizi wa mazingira NEMA na sheria za Wafanyikazi. Makubaliano yetu na Chama cha wafanyikazi wa viwanda vinavyohusika na Kemikali yanaendelea kuzingatiwa na pande zote mbili huku mkataba wa sasa ukimalizika Julai mwaka 2008.

Tunaamini kuwa tuna moja ya maongozi bora zaidi kuhusu HIV na Ukimwi hapa Kenya. Wafanyakazi wetu na waume au wake zao wanapata huduma za bure za kuchunguzwa virusi, kupewa ushauri nasaha na dawa za kuwaongezea maisha wagonjwa. Tunaamini kwamba wakati watu wanapostaafu kutoka kampuni ya Eveready wakiwa na HIV na Ukimwi tunapaswa kuendelea kuwasaidia. Pia tumejumisha marupurupu ya bima yetu ya maisha, bima ya wanaogua magonjwa yasiyotibika kwa urahisi na kusaidia kulipia matibabu ya magonjwa yanayohusiana na HIV na Ukimwi. Pia tunawapa mafunzo wafanyakazi wetu kuhusu HIV na Ukimwi na watoto wa wafanyakazi wetu. Mwaka uliopita tulishuhudia zaidi ya watoto elfu moja na vijana wakipata mafunzo kupitia mradi huu uliodhaminiwa na Eveready. Mnamo mwaka wa 2006 tulitumia karibu shilingi milioni 2.5 kwa miradi mbali mbali ya HIV na Ukimwi. Kwa miradi ya bima ya maisha tulitumia zaidi ya shilingi milioni 4.3 kwa mwaka katika michango ya bima.

Wafanyakazi wetu wa kudumu wana mradi wa marupurupu ya kustaafu na wafanyakazi wanaolipwa mshahara wanao mradi unoachangia marupurupu ya kustaafu. Tuliufunga mradi wa marupurupu ya kustaafu wa mshahara mwezi Oktoba mwaka 2006 ili kuruhusu utaratibu bora wa mchango wa marupurupu ya kustaafu. Tutaendelea kufadhili mpango huu kwa muda wa miaka mitatu ijayo kwa gharama ya takribani shilingi milioni 19 na baada ya miaka mitatu tutafikiria kutekeleza mpango kamili wa mchango wa marupurupu ya kustaafu kwa marupurupu yaliyopatikana kabla ya Oktoba mwaka 2006. Tunachangia takribani asilimia 8.5 ya gharama ya mshahara ili kudumisha marupurupu kwa wafanyakazi wetu.

Wafanyakazi wetu wa kiwanda cha Nakuru wanaendelea kulipwa malipo ya juu kwa viwanda vya sehemu ya Nakuru na ni miongoni mwa wanaolipwa mishahara ya juu ikilinganishwa na viwanda vya Nairobi. Marupurupu ya wafanyakazi wenye mshahara inalingana ifaavyo na masharti ya kikazi kwa kazi wanazofanya.

Kwa shughuli zetu huko Nakuru pia tunatoa huduma za mkahawa zinazotoa mlo kwa wafanyakazi wetu. Wafanyakazi hulipa shilingi 6 pekee kwa kila mlo. Shughuli za manufaa haya hugharimu kampuni shilingi milioni 8 kwa mwaka. Pia tunatoa huduma ya uchukuzi kwa wafanyakazi wa Nakuru bila malipo kwa wafanyakazi wanaohudumu kati ya saa kumi na mbili jioni na saa kumi na mbili alfajiri. Hii huigharimu Eveready takribani shilingi milioni 5.5.

Pia tunaamini katika kuwapa mafunzo wafanyakazi wetu ambayo ni pamoja na ziara za mafunzo kwenye maeneo mengine ya EBC. Mnamo mwaka wa 2006 tulitumia zaidi ya shilingi milioni 5 kutoa mafunzo na kuwastawisha viongozi wetu wa siku zijazo na zaidi ya maafisa 75 walimaliza siku kadhaa katika maeneo mengine ya EBC kwa mafunzo. EBC pia huwatumia maafisa wa mafunzo na wa kiufundi hapa nchini ili kutoa mafunzo na kuimarisha miradi yetu ya huduma za kiufundi. Katika mwaka wa 2006, EBC ilitumia zaidi ya maafisa 200 waliomaliza siku kadhaa kwenye maeneo mbali mbali ya kiufundi. Tulitumia zaidi ya shilingi milioni 300 kwa malipo, marupurupu na miradi mingine ya wafanyakazi mwaka huo.

### **Jukumu la Kampuni kwa Jamii**

Tulitumia karibu shilingi milioni 5 kwenye miradi ya kusaidia jamii tunayohudumia. Hii ni pamoja na shilingi 800 elfu tulizotumia kuelimisha watoto kuhusu HIV na Ukimwi. Shilingi milioni moja kwa msaada wa chakula na shilingi milioni 0.5 kwa visima vya maji. Pia tulitumia karibu shilingi 500 elfu kwa miradi mbali mbali ya kusaidia kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa serikali kuhusu jinsi ya kufahamu athari za bidhaa bandia na zile zisizo halali. Pia tulisaidia miradi mbali mbali inayozingatia watoto, ulinzi wa misitu na maswala ya kinamama. Tumepanga bajeti ya kutumia karibu shilingi milioni 6 kwenye miradi hii mwaka 2007. Hii inawakilisha karibu asilimia 3 ya mapato yetu baada ya kulipa ushuru.

### **Usimamizi wa Kampuni**

Kila mara tumefanya biashara yetu kwa njia ya uwazi. Tuna imani kuu kwamba maadili ya kazi katika viwango vyote vya kampuni yetu ni muhimu. Ikiwa tutapata tatizo la kimaadili litajadiliwa na kamati ya ukaguzi wa hesabu za pesa na Halmashauri inayojumuisha hatua tunazochukua kutatua hali iliyojiri na kwa njia ifaayo tutatoa habari kwa maafisa wanaohusika ili hatua za kisheria kuchukuliwa na wahalifu kushtakiwa.

Tutafanya mabadiliko ya majukumu ya wanachama wa Halmashauri kwenye kamati ya Halmashauri yetu mwaka 2007 kwa kuongezea wakurugenzi wawili watakaokuwa huru. Kamati ya sasa ya Halmashauri ni:-

- Kamati ya Fedha na Usimamizi wa Hatari
- Kamati ya Ukaguzi wa Hesabu za Pesa
- Kamati ya Marupurupu na Uteuzi

Tumeweka maongozi ya maadili ya kikazi na viwango vya tabia kwa wafanyakazi wetu wote na sheria zinazozingatiwa na wafanyakazi wote ndani ya kampuni, zinazopatikana kwenye mtandao wa tovuti yetu. Maongozi haya pia yanahusu maafisa wa kampuni na wakurugenzi. Pia tunatumia kila mwaka kwa wagawaji wa bidhaa zetu maongozi ya maadili ya biashara yetu kwa washirika wa kibiashara na pia kuwomba wafanyakazi wetu kujaza karatasi ya maswali kila mwaka kuthibitisha kuwa shughuli za kazi yao zimetimiza maongozi ya Eveready kwa mwaka uliopita.

Tunaamini katika uendeshaji biashara yetu kulingana na maadili yetu na kwamba hakuna njia za mikato. Lazima tufanye kilicho sawa kila wakati.

### **Utengenezaji Bidhaa**

Mnamo mwaka 2006 tulianza mradi wa kukiimarisha kiwanda chetu. Tunakisia kwamba tutatumia shilingi milioni 50 kila mwaka kwenye mradi huu katika miaka kadhaa ijayo. Mwaka wa 2006, tulitumia jumla ya karibu shilingi milioni 63 kuboresha shughuli za kampuni yetu. Mradi wetu wa kuimarisha kiwanda chetu umegawanywa katika sehemu tatu. Watu, Mfumo na Mitambo. Katika mwaka 2006 tulitumia muda mwingi kushughulikia maswala kuhusu watu na mfumo. Ukadiraji wa mafunzo na utendaji kazi ulitekeleza jukumu muhimu kwani ni lazima tuwe na watu wanaofaa, walio na elimu inayohitajika. Kwa kutumia wataalam wa kiufundi wa EBC tumeanza juhudi za kuegemea utengenezaji bidhaa. Hii inatuhitaji kuchunguza mpango wa kudumisha mitambo yetu na tumeweka hatua madhubuti za kuimarisha udumishaji mitambo yetu katika mwaka 2006 baada ya kuwa na haja ya kukiimarisha kiwanda chetu. Pia tulianza mradi wa ukarabati mkubwa wa mitambo yetu katika sehemu kadha.

Tumeanza kuchunguza shughuli za kiwanda kwa kurejesha kiwango cha utengenezaji bidhaa kinachohtajika. Kwa sasa tunatumia tu asilimia 60 ya mitambo yetu lakini tumepiga hatua ambazo ni pamoja na kuchunguza jinsi tunavyoweza kusimamia wakati kwa rasilimali tuliyo nao. Ni muhimu kuelewa haya ikiwa una mitambo inayofanyakazi kwa saa 24 na kuona ni vipi unaweza kutumia muda wa saa 24 ukitumia mitambo ya kufanyia kazi kama njia ya kihistoria ya kukadiria utendaji kazi. Pia tumeboresha sehemu kadhaa katika kiwanda chetu ili kutoa rasilimali muhimu kwa wafanyakazi wetu. Tutatumia karibu shilingi milioni 6.5 kwa shughuli hizi za uboreshaji kufikia mwisho wa mwaka 2007.

Shughuli muhimu mwaka wa 2007 itakuwa kushughulikia maswala ya mafunzo kwa wafanyakazi wa kiwanda chetu. Lazima tuwianishe ujuzi na hatua za uzalishaji kutoka kwa viwanda vingine vya EBC na kufikia viwango vya Kimataifa.

### **Uuzaji**

Mnamo mwaka 2006 tulishuhudia kupungua kwa mauzo hasa kutokana na sababu zilizojadiliwa hapo mwanzo wa taarifa hii kuhusu matokeo ya mwaka 2005. Wateja wetu

wanapenda bidhaa za bei nafuu na hii ilidhihirishwa kwenye mtindo wetu wa mauzo wa mwaka 2006 pamoja na kupungua kwa bei kwa bidhaa yetu ya 950 blue.

Tunatarajia ukuaji wa juu wa bidhaa yetu kwa wale wasioathiriwa na kupungua kwa mazao na ukame. Pia tunaendelea kutafuta nafasi kwa bidhaa zetu katika masoko ya nje. Tunaendelea kupata nafasi yetu kwenye soko katika nchi za Uganda na Tanzania. Hata hivyo maswala ya Mkataba wa ushuru wa Afrika Mashariki (EAC) yanaendelea kuipendelea Tanzania na kushindwa kwa serikali kuhimiza kuzingatwa kwa viwango vilivyowekwa, ndilo tatizo linalokumba uuzaji bidhaa zetu nje. Hata hivyo biashara ya uuzaji bidhaa nje kwa ujumla inaendelea kukua na tutatumia laini za bidhaa kustawisha masoko hayo. Eveready itatoa suluhisho la kawi ndogo kwa nchi za Afrika Mashariki mwaka huu.

Mnamo mwaka 2006 tulitumia shilingi milioni 60 kwa matangazo ya kibiashara. Miradi yetu inalenga kumpa mteja chaguo la bidhaa aipendayo ili kutimiza mahitaji yake. Tunafahamu juu ya haja ya kutengeneza bidhaa za bei nafuu na hata hivyo ukilinganisha bei za bidhaa zetu na za kampuni nyingine katika sekta ya utengenezaji betri, bei zetu ni sawa. Swala la uwekaji bei linakumbusha kuhusu bidhaa bandia zinazolingizwa kwenye soko la humu nchini kwa njia isiyohalali na bila kulipiwa ushuru ziada wa thamani (VAT) wa asilimia 16 na asilimia 35 kwa njia ifaayo. Tutaendelea kuchunguza hali hii na kutoa habari kwa maafisa wa serikali wanaohusika ili hatua zichukuliwe.

Tutasherehekea mwaka wetu wa 40 mwaka 2007 na hii itashirikisha shughuli zetu za matangazo kwa mwaka 2007.

### **Fedha**

Mwaka wa 2006 ulikuwa na changamoto nyingi. Kulikuwa na ukame kwenye nusu ya kwanza ya kipindi cha matumizi ya pesa, uliosababisha kupungua kwa uwezo wa ununuzi kwa mteja na kusababisha kupungua kwa mauzo ya betri. Hali hii ilizidishwa na ongezeko la bei za mali ghafi na hasa zinki kwa viwango vya juu mno na kusababisha shinikizo la mashindano kutoka kwa bidhaa za bei duni.

Licha ya changamoto hizi, wasimamizi walibuni hatua za kukabiliana na changamoto hizi. Hatua hii ilifikiwa kwa kutekeleza mbinu ya kuweka bei nafuu ili kudumisha nafasi yetu kwenye soko pamoja na ukuaji katika utoaji bidhaa bora na mauzo ya nje. Vile vile, wasimamizi walifikia hatua za uthibiti kwa gharama za utendaji kazi katika mwaka huo. Matumizi ya ziada ya kampuni yalithibitiwa mwaka 2005 na 2006.

Mnamo mwaka wa 2006 tulianza mpango wa kuunganisha na kujumuisha shughuli zetu kwenye mtandao wa kompyuta kati ya Nakuru na Nairobi. Hii ilihusisha mabadiliko ya mfumo wa simu uliopunguza gharama. Tunatumaini kwamba mradi huu wa uunganishaji shughuli zetu utakamilika kufikia mwisho wa mwaka 2007. Hii pia ni pamoja na kuimarishwa kwa orodha ya malipo ya mshahara kwa kutumia teknolojia ya BIO kwa kazi za kazi za kunakili wakati viwandani.

Mauzo yetu mwaka 2006 yalikuwa shilingi bilioni 2 na faida baada ya kulipa ushuru ya shilingi milioni 166 ikilinganishwa na shilingi bilioni 2.2 na shilingi milioni 187 mwaka uliotangulia.

### **Mwisho**

Ninajivunia sana kampuni yetu na ukuaji ulioshuhudia miongoni mwa watu wengi mwaka wa 2006. Bado tunakabiliwa na changamoto za kawaida katika biashara yetu lakini upunguzaji gharama ya utengenezaji bidhaa ni lazima. Gharama ya utengenezaji bidhaa hapa Kenya inaendelea kuwa ya juu ikilinganishwa na maeneo mengine ya EBC. Gharama ya mali ghafi inaendelea kuwa ya juu kuliko maeneo mengine ya EBC kutokana na gharama za uchukuzi humu nchini (kutoka Mombasa hadi Nakuru). Pia tumeathiriwa na ongezeko la ushuru kwenye kampuni yetu ambalo halijajumuishwa katika nchi nyingine.

Mwaka wa 2006 tulikuwa na mzigo zaidi wa ongezeko la bei ya zinki kutoka dola 1,700 hadi zaidi ya dola elfu 4 kwa tani moja ambayo ni asilimia 30 ya gharama ya betri. Hatuwezi kuongeza bei zetu kwa kiwango cha juu sana ili kufidia ongezeko la bei ya zinki na tulilazimika kutumia shilingi milioni 30 kwenye ongezeko hili katika kampuni. Iwapo mashindano ni halali au si halali, bado ni mashindano na lazima tuyashughulikie ili kulinda malengo ya biashara yetu ya muda mrefu. Tutaendelea kuiomba serikali kubuni mazingira sawa na ya maadili ya kibiashara.

Hatujapata mabadiliko ya malalamiko ya kisheria tunayohusika nayo. Tunaendelea kuamini kwamba hatujasababisha hasara ya kiafya na visa vya wafanyikazi viwandani. Visa vingi vimecheleweshwa na mahakama au walalamishi katika mwaka wa 2006. Tuna imani kuu kuhusu msimamo wetu na mawakili wetu wanaendelea kuwa na imani kwamba tunayo nafasi ya ufanisi katika malalamishi yaliyowasilishwa na hakuna malipo maalum ya fidia yaliyotengwa. Tuna beba mzigo wa bima ya afya na usalama kwa malipo yote ya bima ya kampuni. Hatuna malipo ya bima ya kima cha shilingi milioni 163 kwa visa vya tangu mwaka 1995.

Lengo letu mwaka 2007 ni kuongeza laini za mauzo kwa uimarishaji wa shughuli zetu. Ni wazi kwamba ni lazima tukusaidie kwa matokeo ya mapato bora mwaka hadi mwaka. Tunakuomba pia utusaidie na hii inamaanisha kuwa familia na marafiki wanatumia bidhaa zetu. Pia ni muhimu kutumia bidhaa zilizotengenezwa hapa nchini ikiwa zinapatikana. Tuna wastawisha wagawaji kadhaa wa humu nchini kugawa bidhaa mbali mbali za mali ghafi ambazo tumeagiza kwa miaka mingi kutoka nje na tunatarajia kuwa kampuni hizi za Kenya zitaidhinishwa kufikia mwisho wa mwaka 2007 ili kuisambazia kampuni ya Eveready mali ghafi na pia kusambazia maeneo mengine ya EBC.

